



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MUDA KWA MKUSANYA TAARIFA MSAIDIZI
KWENYE ZOEZI LA ANUANI ZA MAKAZI**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Musoma anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi ya wakusanya taarifa wasaidizi kwenye zoezi la Anuani za makazi katika **Kata** na **Mitaa** Halmashauri ya Manispaa ya Musoma

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- i. Awe anamiliki simu janja (android) yenye uwezo wa kukaa na na chaji kwa siku nzima ikiwa kwenye internet
- ii. Awe mkazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma
- iii. Awe na barua pepe email na nywila (password) inayofanya kazi
- iv. Atoke kwenye mtaa husika hivyo ikiwezekana barua za maombi zipitishwe na mtaa
- v. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18-35

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja, na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anuani za makazi
- iii. Kutuma data kwenye mfumo wa anuani za makazi

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;-

- i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- ii. Picha (passport size 2)
- iii. Hakikisha unaandika namba zako za simu ya mkononi

D. MALIPO

Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe zikiwa na anuani kamili ya mwombaji , namba ya simu, barua pepe na ziwasilishwe ofisi ya mkurugenzi wa manispaa kwa anuani ifuatayo;-

MKURUGENZI WA MANISPAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

S L P 194

MUSOMA

Mwisho wa maombi ni tarehe 20.3.2022 saa kumi jioni

BOSCO .O. NDUNGURU
MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA.